# OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA

**SHULE YA SEKONDARI LUHUWIKO,**
**S.L.P 245,**
**MBINGA.**

**___/12/2020**

**Kumb.Na. LSS/JI/VOL.01/01/02**
**Jina la mwanafunzi.........................................**
**K.K MZAZI/MLEZI...............................................**
**S.L.P............................**

## FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI LUHUWIKO.

## A: UTANGULIZI.

Shule ya sekondari ni shule ya umma, ni shule ya wanafunzi mchanganyiko (wanafunzi wa kike na wa kiume) pia ni shule ya kutwa. Shule ya sekondari Luhuwiko inapatikana katika kata ya Luhuwiko halmashauri ya Mbinga Mji,shule ipo umbali wa kilomita 2 kutoka katikati ya mji wa Mbinga na kilomota moja toka stendi ya Sepukila barabara ya Songea Mbamba Bay. Shule ina namba ya usajili **S. 5151** na namba ya mtihani **S. 5892.** Uongozi wa shule unapenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuwa miongoni mwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021, ni matumaini yetu utakuwa na nidhamu nzuri na utatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule, pamoja na masharti yote ya kujiunga na shule kama ilivyoorodheshwa katika fomu hii.

***SCHOOL MOTTO:*** *EDUCATION FOR STANDARD, CHALLENGE IS YOUR SELF. (ELIMU KWA VIWANGO, CHANGAMOTO NI WEWE).*

***SCHOOL VISION:*** ENABLE STUDENTS TO ACHIEVE BETTER EDUCATION AND TO BECOME POTENTIALS IN FUTURE

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 na unatakiwa kufika siku hiyo ukiwa na mahitaji yote yaliyoainishwa.

## B: SARE ZA SHULE KWA WASICHANA.

1. Sketi mbili zenye marinda ya kawaida za rangi ya **BLUE NELLY** ndefu zifike kwenye kisigino.
2. Tai mbili ndefu za kufunga za rangi ya BLUE NELLY.
3. Blauzi mbili nyeupe (TETRONI) za mikono mifupi.
4. Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi, visiwe na visigino virefu pia vya kufunga kwa kamba.
5. Jozi mbili za soksi nyeupe.
6. Sweta la rangi ya **DARK BLUE** lenye shingo ya V na upinde (Lenders) shingoni na mikononi.
7. Anatakiwa awe na nywele fupi zinazotunzwa vizuri na zisizotiwa dawa.
8. Raba kwa ajili ya michezo (NI LAZIMA).
9. Hijabu kwa waislamu kitambaa rangi nyeupe. (Kwa Waislamu pekee).
10. Nguo rasmi za michezo (Track suit) za rangi ya Blue (NI LAZIMA).

## C: SARE ZA SHULE KWA WAVULANA

1. Suruali mbili zenye Turn up na pindo la chini ,zenye upana wa kutosha za rangi ya **BLUE NELLY**
2. Tai mbili ndefu za kufunga za rangi ya BLUE NELLY.
3. Shati mbili nyeupe (TETRONI) za mikono mifupi.
4. Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi, visiwe na visigino virefu pia vya kufunga kwa kamba.
5. Jozi mbili za soksi nyeusi.
6. Sweta la rangi ya **DARK BLUE** lenye shingo ya V na upinde (Lenders) shingoni na mikononi.
7. Anatakiwa awe na nywele fupi zinazotunzwa vizuri na zisizotiwa dawa.
8. Raba kwa ajili ya michezo (NI LAZIMA).
9. *Nguo za michezo (Bukta na T shirt ) rangi ya bluu* (LAZIMA)
10. Mkanda wa suruali wa rangi nyeusi wa ngozi.
11. Nguo rasmi za michezo (Track suit) za rangi ya Blue (NI LAZIMA).

**MUHIMU**: Kila mwanafunzi ajiandae kikamilifu na kuwa na mahitaji ya muhimu ya darasani kama vile:- Daftari kubwa 22 (daftari 11 za nukuu (notes) na nyingine 11 za mazoezi na masahihisho ya mitihani), kalamu za wino za kutosha, mathematical set, begi la kubebea daftari, pia inashauriwa uwe na vitabu mbalimbali vya masomo, pia kamusi (dictionary) ambayo itakaguliwa pindi mwanafunzi atakaporipoti shuleni na hatapokelewa ikiwa hana mahitaji haya ya msingi.

**VIFAA VINGINE VYA KUJA NAVYO UNAPORIPOTI SHULENI.**

i/ Fagio moja la kufagilia (CHELEWA).
ii/Ndoo ndogo moja mpya na safi
iii/ Jembe moja jipya lenye mpini wake.
iv/ Fyekeo moja

**D: MENGINEYO.**

Mwanafunzi atambue lugha rasmi ya mawasiliano, kufundishia na kujifunzia kwa masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili ni Kiingereza, hivyo unapaswa kuchukua kujifunza lugha hiyo mapema na kwa weledi mkubwa ili uweze kuwa na mawasiliano bora uwapo shuleni.
Pia endapo mwanafunzi hatofika shuleni ndani ya siku 90 baada ya tarehe ya kufungua shule atakuwa amedharau agizo la serikali, aidha hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mzazi wa mwanafunzi husika.
Kama mtoto wako ameenda kujiunga na masomo katika shule za binafsi tafadhali unapaswa kutoa taarifa za maandishi mara moja kwa uongozi wa shule ambayo mtoto wako amechaguliwa.

**E: SARE ZA SHULE.**

Unapaswa kuwa na sare ya shule mshono uliokubaliwa na kwa wakati kama ilivyopangwa kwa:-

i/Wakati wote wa masomo.
ii/ Safari zote za nje ya shule kwa jina la shule.
iii/ Wakati wa kwenda hospitali.
iv/ Wakati wa maandamano.
v/ Unapaswa kuvaa nguo za michezo na za kazi za mikono kama utakavoelekezwa.

**F: MIPAKA YA SHULE.**

i/ Unapaswa kufahamu mipaka yote ya shule na huruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mkuu wa shule wakati wote wa masomo.

ii/ Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea nyumba za walimu, ofisi, maabara, na na wafanyakazi wasio walimu bila kibali cha mkuu wa shule.

iii/ Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea maeneo yafuatayo:-

a) Vilabu vya pombe.
b) Majumba ya starehe.
c) Majumba ya kufikia wageni (Guest Houses).

**G: MAKOSA YANAYOWEZA KUPELEKEA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Uvutaji wa bangi na aina nyingine za madawa ya kulevya.
3. Uharibifu wa makusudi wa mali.
4. Kuoa au kuolewa.
5. Utoro wa shule kwa muda mrefu (siku 90 mfululizo).
6. Uasherati.
7. Makosa ya jinai.
8. Kupata mimba au kumpa mimba msichana ndani na nje ya shule.
9. Ulevi wa aina yoyote.
10. Kupigana.
11. Kudharau bendera ya Taifa.
12. Kutoa mimba.
13. Utovu wa nidhamu kwa ujumla.
14. Kashfa dhidi ya uongozi wa serikali, dini au uongozi wake.
15. Mwanafunzi kumiliki simu ya mkononi.

**H: USAFI.**

Usafi ni wajibu wa kila mwanafunzi kama sehemu ya maisha yake ya kila siku, hivyo utashughulikia:-

i/ Usafi binafsi wa mwili na mavazi ukiwa umevaa sare nadhifu muda wote inapohitajika.

ii/ Usafi wa maeneo yafuatayo:- Ukumbi wa mikutano, madarasa, vyoo, maabara, maofisi, viwanja, na barabara.

**I: MAHUDHURIO.**

Kuthamini muda wa kuwepo mahali unapotakiwa kwa mujibu wa ratiba au maelekezo kutoka kwa uongozi wa shule.

i/ Kuwahi kufika shuleni na kudumu muda wote kama ratiba inavyoonesha.

ii/ Kuwepo shuleni kwa siku zote za masomo isipokuwa kama kuna sababu za msingi zitakazopelekea ushindwe kufanya hivyo.

iii/ Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa ikiwemo vipindi vya dini kila wiki.

iv/ Kushiriki kazi zote za mikono na michezo kama itakavyoelekezwa kwenye ratiba.

v/ Kuhudhuria mikutano yote ya shule mfano Baraza la shule, ukaguzi na usafi, kupandisha bendera ya Taifa, maandamano halali, vikao vya madarasa , na kushiriki shughuli mbalimbali za vikundi kama vilabu vya masomo, dini, michezo, utamaduni na maadili.

vi/ Kuitikia miito ya dharura mara moja pindi inapotokea.

**J: MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILIHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hiyo itakabidhiwa shuleni kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutokushiriki kaika migomo, fujo na makosa mengine ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**L: Tafadhali soma kwa makini maelekezo na maagizo na kuyatekeleza kikamilifu.**

## KARIBU SANA LUHUWIKO SEKONDARI.

..............................

**WILSON E. KALIKUMBI**
**MKUU WA SHULE.**
**SIMU:0763802803**

THE HEADMASTER
LUHUWIKO SEC. SCHOOL
MBINGA TC.